Kitabu cha Yoshua

MAZINGIRA
Kitabu cha Yoshua kinahusika zaidi na Waisraeli walipoteka nchi ya Kanaani na nchi hiyo ilivyogawiwa kati ya makabila yake. Tangu wakati wa Ibrahimu Mungu alikuwa ameahidi kwamba Kanaani ingekuwa mali ya Waisraeli (Mwa 13:14-17), lakini karne kadhaa zilipita mpaka Waisraeli walipokuwa taifa kubwa la kutosha kwa kuteka na kumiliki nchi hiyo.

Taifa la Israeli lilikua na kuongeza hasa katika nchi ya Misri, na wakati wa Mungu ulipowadia, Musa aliwaongoza watu hao kutoka Misri kuelekea Kanaani (Kut 3:7-10; 12:40-41). Lakini watu walipofika karibu na Kanaani ambapo wangeweza kuandaa mashambulio, waliwaogopa Wakanaani wakamwasi Mungu. Kwa ukaidi wao, watu walikataa kumtegemea Mungu na kuingia Kanaani, isipokuwa viongozi wawili, yaani Yoshua na Kalebu. Mungu akawaadhibu jangwani mpaka watu wazima (waliokuwa na miaka 20 na kuzidi, isipokuwa Yoshua na Kalebu) walipokufa na kizazi kipya kilipokuwa na nguvu ya kutosha (Hes 14:28-35). Wakati huo, miaka 40 baada ya wazazi wao kuondoka Misri, watu wa kizazi kile kipya walikuwa tayari kuingia Kanaani. Kambi yao kubwa ilikuwa mashariki mwa Mto Yordani kukabili Yeriko (Hes 22:1). Musa alikuwa amekufa kabla ya muda mfupi (Kum 34:1-5), na Yoshua alikuwa kiongozi mpya wa taifa hilo (Kum 34:9; Yos 1:1-2).

Kiongozi mpya wa Israeli
Yoshua alizaliwa na kukulia Misri akiwa mtumwa, lakini miaka ya taabu huko Misri ilimsaidia kujenga tabia, uwezo na imani ya kumtegemea Mungu ambayo siku moja ingemfanya awe mtu wa maana sana katika taifa lake. Muda mfupi baada ya Waisraeli kuondoka Misri, Yoshua alionyesha uwezo wake wa kuongoza alipokusanya kwa haraka sana jeshi dogo na kuwafukuza wachokozi Waamaleki (Kut 17:8-16). Waisraeli walipofika Mlima Sinai, Yoshua alikuwa msaidizi maalumu wa Musa. Yeye peke yake alifuatana na Musa walipokwea mlima, ambapo Musa alikutana na Mungu katika wingu, lakini Yoshua alibaki nje yake (Kut 24:13). Vile vile Yoshua hakutoka katika hema ambamo Musa alikutana na Mungu (Kut 33:11; taz. Hes 11:28).

Siku moja, Waisraeli walipomwasi Mungu jangwani, Yoshua alionyesha imani yake yenye ujasiri amapo yeye na Kalebu walisimama imara kinyume cha wenzao wote (Hes 14:9). Imani yake ya kumtegemea Mungu ilimpa uvumilivu na kumlinda asije akachukuliwa na tamaa ya ubinafsi ya kutaka makuu. Hakuwa na wivu dhidi ya Musa kuwa kiongozi wa Israeli, bali alijaribu kumtetea watu wengine walipojaribu kushambulia daraja lake la pekee (Hes 11:26-30).

Mungu alimchagua Yoshua awe kiongozi wa taifa baada ya Musa, lakini alionyesha wazi kwamba Yoshua asingekuwa na mamlaka makubwa sawa sawa na Musa. Hali ya Musa ilikuwa ya pekee naye alisema na Mungu ana kwa ana. Lakini baada ya kufa kwake, uongozi wa kiraia na ule wa kiroho ungekuwa juu ya watu tofauti. Tangu wakati huo kawaida yake ilikuwa kwamba, kiongozi wa kiraia alipata maagizo ya Mungu kwa njia ya kuhani mkuu (Hes 27:18-23). Hata hivyo, Yoshua alikuwa mtu aliyemwelewa Mungu. Uzoefu wake kama kiongozi wa kiroho, mtawala wa kiraia na mkuu wa jeshi ulimfaa sana kuwaongoza Waisraeli katika nchi yao mpya na katika wakati mpya uliowakabili (Kum 31:7, 14, 23; 34:9).

Mtindo wa Kitabu cha Yoshua
Kitabu cha Yoshua kimepata jina lake kutokana na mtu ambaye habari zake zimesimuliwa zaidi humo, lakini hakimtaji mwandishi wake. Inawezekana kwamba mwandishi alipata habari nyingine kutokana na kumbukumbu ambazo Yoshua mwenyewe aliziandika (Yos 24:25-26) na habari nyingine kutokana na vitabu vingine vya historia vya wakati ule (Yos 10:13). Habari nyingine pia aliweza kupata kutokana na ripoti za kikabila na kitaifa kuhusu mahali, koo na matukio mbalimbali (Yos 18:8-9).

Ingawa kitabu kinaeleza mateka ya nchi ya Kanaani, hakitoi orodha ya kinaganaga kuhusu matukio yote ya historia. Vita vya kuteka Kanaani vilichukua muda mrefu (Yos 11:18) usiopungua miaka mitano (Yos 14:7, 10), lakini mwandishi alitaja baadhi ya vita virefu katika mistari michache tu, na mambo mengine yasiyokuwa na maana sana ya kivita aliyaandika kirefu.

Sababu ya tofauti hizo katika masimulizi ni kwamba, madhumuni maalumu ya mwandishi hayakuwa kuandika ripoti ya kinaganaga kuhusu vita na siasa, bali alitaka kuonyesha kazi ya Mungu na watu wake. Mwandishi alikuwa mhubiri kuliko mwandishi wa ripoti na orodha mbalimbali tu. Alikuwa nabii kuliko mwandishi wa hisroria.

Kwa Waisraeli kazi ya kwanza ya nabii haikuwa kutabiri mambo ya usoni, bali alikuwa mtu aliyewajulisha watu mapenzi ya Mungu (Isa 1:18-20; Yer 1:7,9; Amo 3:7-8; taz. Kut 4:10-16; 7:1-2). Wao waliona historia yao kama ufunuo wa matendo ya Mungu, na kwa sababu hii vitabu vingi vya Biblia tunavyoviona vya historia, Waisraeli waliviita vya unabii. Waandishi wengi wa historia katika Israeli walikuwa manabii (1 Nya 29:29; 2 Nya 9:29; 12:15).

Waisraeli waligawanya vitabu vyao vya unabii katika sehemu mbili zilizoitwa Vitabu vya Unabii wa Kwanza (Yoshua, Waamuzi, Samweli na Wafalme), na Vitabu vya Unabii wa Baadaye (Isaya, Yeremia, Ezekieli na vitabu 12 vya manabii wadogo). Katika vitabu vya Unabii wa Kwanza, Mungu alidhihirisha makusudi yake kwa njia ya historia ya Waisraeli, na kwa kweli mataifa yote yalikuwa chini ya utawala wake mkuu. Katika vitabu vya Unabii wa Baadaye, Mungu alidhihirisha makusudi yake zaidi kwa njia ya maneno ya wasemaji wake.

Kwa sababu ya njia hii ya pekee ya Waisraeli kutazama historia, mwandishi wa kitabu cha Yoshua hakujaribu kuorodhesha kila tukio lililotokea wakati ule, wala hakuandika katika utaratibu maalumu wa mfululizo wa matukio. Zaidi alichagua na kupanga mambo yake kadiri ya kusudi lake kuu la unabii. Alitaka kuwasaidia watu wamjue Mungu zaidi, akishughulika na matukio yale yaliyokuwa na maana kubwa katika uhusiano wa taifa na Mungu wake.

MUHTASARI

1:1-5:15	Kuingia Kanaani
6:1-12:24	Kuteka nchi
13:1-22:34	Kugawanya nchi
23:1-24:33	Yoshua anaaga